**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

SOMO LA INNE KATIKA

# "Tuijuwe njiya ya wokovu"

## KWA KUJIFUNZA NA KUTII NENO LA MUNGU KWA KUTARAJIA UZIMA WA MILELE

**Utangulizi**

*Mpendwa katika Kristo, ufuatao ni mfululizo wa masomo manane ambayo imeandaliwa kwa wakristo walio na nia ya kujuwa mambo ya muhimu kuhusu wokovu (kuufikiya na kuulinda) kwa nia ya kuepuka maangamizi ya milele inayotarajiwa kwa wale wasiojali neema kubwa Mungu alitupa kwa njiya ya Yesu Kristo.*

*Masomo haya yana mada zifuatazo:*

Somo la 1: Maisha bila Kristo
Somo la 2: Wokovu kwa njiya ya Kristo
Somo la 3: Mamlaka ya Kristo
Somo la 4: Imani katika Kristo
Somo la 5: Toba kwa jina la Kristo
Somo la 6: Ubatizo katika Kristo
Somo la 7: Kanisa la Kristo
Somo la 8: Maisha mapya katika Kristo

*"Na Filipo aliendа mahali alipo na kumsikia yule mtu anasoma kitabu cha nabii Isaya. Filipo akamwuliza, "Je, unaelewa maneno hayo unayoyasoma?" Yule towashi akasema, "Nitawezaje kuelewa pasipo mtu kunifafanulia?" Hivyo akamsihi Filipo ili apande na kuketi pamoja naye"* (Mdo. 8:30-31).

*"Hivyo kwa mwaka mzima Barnaba na Sauli wakakutana na kanisa na kufundisha idadi kubwa ya watu. Ilikuwa ni katika kanisa la Antiokia kwa mara ya kwanza wanafunzi waliitwa 'Wakristo.'"*(Mdo. 11:26).

*"Lakini baadhi yao kwa ukaidi walipokataa kuamini na kukashifu ujumbe wake mbele ya umati wa watu, Paulo aliachana nao, akawachukua wanafunzi na kuhojiana nao kila siku katika darasa la mtu mmoja aitwaye Tirano"*(Mdo 19:9).

*"Watu hawa walikuwa wema kuliko wale wa Tesalonika, kwa sababu walipokea Neno kwa nia iliyokuwa tayari kabisa, wakatafuta Maandiko kila siku kujuwa hakika ya maneno yale (waliofunzwa)"* (Mdo. 17:11).

*Mungu akubariki na kukuumbiya imani safi, juhudi na moyo wa utiifu kwa haya unayoyasoma.*

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

# **Somo la inne:** Imani katika Kristo.

Injili inafundisha wazi kwamba, kuokolewa toka katika dhambi ni lazma watu wawe na imani (waamini) katika Mungu na katika Yesu Kristo. "*Msifadhaike myoyoni mwenu. Mnaamini Mungu, mniamini mimi pia*" (Yohana 14:1). Katika Yohana 6:47, Neno linasema hivi: "*Kweli, kweli ninawaambiya ninyi, yeye mwenyi kuniamini ana uzima wa milele*". Tena tunaposoma katika Yohana 11: 25-26 ukweli ufuatao: "*Yesu akamwambia, "Mimi ndiye huo ufufuo na uzima. Yeye aniaminiye Mimi, hata akifa atakuwa anaishi na ye yote aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je, unasadiki haya?*". "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza Mungu, kwa maana ye yote anayemjia Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko na ya kuwa huwapa thawabu wale wamtafutao kwa bidii.*" (Waebrania 11:6). Yesu alisema wazi : « *Niliwaambia kuwa mtakufa katika dhambi zenu, kwa maana msipoamini ya kwamba 'Mimi Ndiye,' mtakufa katika dhambi zenu* » (Yohana 8:24). "*Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.*" (Yohana 3:16). "*Kwa hiyo ndugu zangu, nataka ninyi mjue kwamba kwa kupitia huyu Yesu msamaha wa dhambi unatangazwa kwenu. Kwa kumpitia yeye, kila mtu amwaminiye anahesabiwa haki kwa kila kitu ambacho asingeweza kuhesabiwa haki kwa sheria ya Musa.*" (Matendo 13: 38-39). Soma tena Marko 16:15, 16; Yohana 6:29, 11:25-27, 12:36, Matendo 10:43, 15:9, Warumi 1:16, 3:25-26, Waefeso 2:8.

Kwa kuwa Yesu Kristo ni zawadi ya Mungu kwa ulimwengu na Mwokozi wa pekee, tunataka kusisitiza katika nakala hii, imani katika yeye. Basi tuzingatie umuhimu wa imani katika Kristo, kama ilivyofunuliwa katika Injili.

## ***1. Kukubali ukweli kwamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu.***

Hii ndiyo maana ya imani katika Kristo kama vile Injili inatufundisha. Hakuna kati yetu aliyewahi kuona Kristo katika hali yake ya mtu. Hata hivyo, tunaamini na kumkubali kama Mwana wa Mungu na Mkombozi wa watu, kama Mwokozi wa ulimwengu, aliyesulibiwa na kufufuka.

Kwa nini tunayaamini bila shaka? Kwa sababu ya ushuhuda au ushahidi unaotolewa kwetu na Injili ya Yesu Kristo. Waebrania 11:1 inatupa sehemu ya tafsiri ya imani kusema kwamba ni "udhabiti" wa mambo yasiyoonekana. Hakuna mmoja kati ya walio hai leo ambaye amewahi ona mfalme Farao, lakini tunakubali kuwepo kwake kwa sababu ya ushahidi usioweza kupingwa wa historia. Sisi kamwe kuona Yesu katika hali ya mtu au kuona na macho yetu kazi zake za ajabu,

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

lakini tuna ushahidi, kupitiya Injili, kuhusu kila kitu amefanya kwa ajili yetu. "*Basi ndugu zangu nataka niwakumbushe kuhusu Injili niliyowahubiria, mkaipokea na ambayo katika hiyo mumesimama. Kwa Injili hii mnaokolewa mkishikilia kwa uthabiti neno nililowahubiria ninyi. La sivyo, mmeamini katika ubatili. Kwa maana yale niliyopokea ndiyo niliyowapa ninyi, kama yenye umuhimu wa kwanza: Kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yasemayo Maandiko, ya kuwa alizikwa na alifufuka siku ya tatu*" (1 Wakorintho 15:1-4).
Hakuna njia nyingine ya kuwa na imani katika Kristo isipokuwa tu kwa ushuhuda wa Injili, Neno la Mungu lililofunuliwa kwetu kupitiya Yesu Kristo na mitume wake. "*Basi, imani huja kwa kusikiya, na kusikia huja kwa Neno la Kristo.*" (Warumi 10:17). "*Petro alisimama na kusema: "Ndugu zangu, mnajua kwamba siku za kwanza Mungu alinichagua ili kwa midomo yangu watu wa Mataifa wapate kusikia ujumbe wa injili na kuamini*" (Matendo 15 : 7). Soma Yohana 17:20, 20:30-31, Matendo 17:11-12.

Lakini tujuwe kwamba, ili mtu aokolewe, haitoshi tu kukubali ukweli kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu na Mwokozi wa ulimwengu. Katika Yohana 12:42-43 tunasoma juu ya baadhi ya watu ambao waliamini Yesu, lakini wao hawakmkiri kwa kinywa: "*Lakini wengi miongoni mwa viongozi wa Wayahudi walimwamini, lakini kwa sababu ya Mafarisayo hawakukiri waziwazi kwa maana waliogopa kufukuzwa katika masinagogi. Wao walipenda sifa za wanadamu kuliko sifa zitokazo kwa Mungu*". Na Mathayo 10:32-33 anasema : "*Kila mtu atakayenikiri mbele ya watu, mimi nami nitamkiri yeye mbele za Baba yangu aliye mbinguni. Lakini ye yote atakayenikana mimi mbele ya watu, mimi nami nitamkana mbele ya Baba yangu aliye mbinguni.*"

Ingelikuwa imani tu katika Kristo ndiyo inatosha kwa kutuokoa sisi, basi mapepo pia wangeliokolewa kwa sababu wanaamini pia, kama alivyoandika Yakobo : "*…mashetani wanaamini vilevile na kutetemeka*" (Yakobo 2:19).
Kumbuka, hata hivyo, kwamba ni lazima mtu aje kwa Bwana, kwa ajili ya wokovu wetu, na kwamba hakuna mtu atakuja kwake ikiwa hasadiki ukweli ambao Injili inaeleza kuhusu Yeye. Sehemu ya kwanza ya mstari wa Waebrania 11:1 imefafanua imani kama « *uhakika wa mambo yatarajiwayo* ». Neno "uhakika" hutafsiriwa mara nyingine kama « tegemeo » au tena kama « msingi ». Basi, imani ni msingi na tegemeo la matumaini. Kama mtu haamini Kristo, yeye hana msingi wala tegemeo kwa ajili ya tumaini la wokovu katika Yesu. Hivyo tunaona haja kamili ya kuamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu aliye hai na pia ana uwezo wa kutuokoa kutoka katika dhambi zetu.

## *2. Kuwa na matumaini katika Kristo*

Je, inawezekana mtu kuamini ukweli wote wa Injili na kushindwa kuweka matumaini yake kamili ndani ya Kristo kwa ajili ya wokovu? Hakuna msingi wala tegemeo kwa ajili ya tumaini la wokovu katika Kristo bila kuwa na matumaini kamili ndani yake. Hakika, hakuna mtu atakaye tafuta wokovu ndani yake ikiwa hana kwanza matumaini ndani yake. Hivyo ni wazi kwamba, imani iwahesabiyao waumini haki na iokowayo, ni zaidi ya imani itamkwayo tu, kwa sababu ndani

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

kuna uhakikisho binafsi kwamba Yeye anauwezo wa kutuokowa na hiyo haja ya kuona tunakombolewa kutoka utumwa wa dhambi zetu kwa uwezo wake mkubwa wa kiMungu.

**3. Kumtii Kristo.**

Imani tupu katika Kristo hayitoshi kwa kufikiya wokovu, isipoambatana na kutii neno lake. Jinsi gani matumaini ya wokovu katika Kristo yanaweza kuwa na kiini ikiwa hatumtii ? Yesu alisema, "*Kwa nini mnaniita, 'Bwana, Bwana,' nanyi hamfanyi ninayowaambia?*" (Luka 6:46). Tena tunasoma: "*Si kila mtu aniambiaye, 'Bwana, Bwana,' atakayeingia katika Ufalme wa Mbinguni bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni*" (Mathayo 7:21). Petro anasema: *"…mumejitakasa nafsi zenu kwa kuitii ile kweli …*" (1 Petro 1:22). Tunasoma katika Yakobo 2: 24: "*Munaona ya kama mtu anahesabiwa haki kwa matendo yake pia wala si kwa imani peke yake.*" Soma pia Warumi 6:17-18.
Hivi vifungu ambavyo hutufundisha kwamba wokovu hupatikana kwa kutii Neno la Kristo, havitangukani na mafundisho yanayodai kuwa wokovu hupatikana kwa njiya ya imani kwa sababu ni kukubali ya kamba Yesu Kristo ni mwana wa Mungu na mkombozi wa wale ambao wanamtegemea kwa kufikiya wokovu, na hii imani ndio msingi wa kila utiifu wa mpango wa wokovu. Mbele mtu aamini, lazima asikiye kwanza na baadaye anatimiza yaliyo katika Neno, yaani matendo yake ya utiifu yanahitajika wala si kuamini kwa midomo tu. Kwa mifano zaidi kuhusu kuamini na kutii, soma Waebrania 11:7; 11:17. Kumbuka kwamba Mungu huwapa tu baraka za neema yake wale watiifu kwa mapenzi na maagizo yake. Soma kwa makini Waebrania 11:4-38.

Yakobo (Sura ya 2:19-20) anasisitiza sana akiunganisha imani na utiifu wala tena matendo ya imani. Kumbuka kwamba wale wasioamini hawana ahadi zaidi kuliko pepo "*Unaamini kwamba kuna Mungu mmoja. Vema! Hata mashetani yanaamini hivyo na kutetemeka. Je, wataka kujua, wewe mwanadamu usiye kitu, kwamba imani bila matendo haifai kitu?*" Endelea kusoma Yakobo 2:14-26.

Ni makosa kudhani kwamba baadhi ya mafundisho yanayosema kwamba wokovu kwa njia ya imani katika Kristo lazima yaonekane katika matendo ya utiifu, eti ni kinyume na vifungu vile kama Waefeso 2: 8-9, vinavyosema kuwa "*Kwa maana mumeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, wala neno hili halikutoka ndani yenu wenyewe, ni zawadi kutoka kwa Mungu. Si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.*" Kutoa hitimisho kwamba kifungu hiki hufundisha tu kuuhusu kuhesabiwa haki kwa imani peke yake, ni kutokuelewa vizuri ni matendo gani aliyosema Yesu na ni yale ndiyo wanadamu wapashwa kutii kwa kuufikiya wokovu. Tukumbushe kwamba mahali pengine, mtume Paulo anasema kuhusu "*matendo ya haki tuliyoyafanya*" (Tito 3: 5) na juu ya hayo wengine wangejaribu kuweka msingi wa wokovu wao. Hizi kazi (haya matendo), zilihitaji imani na hata kifo cha Kristo. Lakini sasa, wakati aliyekuwa mwenye dhambi anatimiza matendo (hatua) yanayohitajika (zinazohitajika) katika "tume kubwa" (kwa kifransa *la Grande Commission*); yaani kuamini, kutubu, kubatizwa; hategemeyi matendo yake binafsi wala hatimizi desturi za wanadamu bali mapenzi ya Kristo wakati alipowatuma mitume wake. Basi, yeye anayekataa kushuhudiya imani yake ili atii mapenzi ya

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

Mungu, yeye bila shaka, amedharau hata neema ya Mungu: yeye si mtiifu wa neno la Kristo.
Neno "imani" na kisawe (synonyme) chake "sadiki", linaloelekeya mambo ambayo Mungu ameamuru wale ambao wanahaja ya kutoka katika maisha ya dhambi, ni namna ya masemi inayomruhusu mtu aseme sehemu moja ya kitu kwa kumaanisha kitu kizima. Tunajua kwamba imani, katika maana yake fupi, inayomaanisha kukubali Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu aliye hai, Bwana na Mwokozi, ni sehemu wala hata maelezo kwa ufupi wa "mpango wa wokovu" (*le Plan du Salut*). Na kwa sababu imani hii, inapounganishwa na matumaini na huo utiifu unaohitajika na Bwana, inatumiwa kwa kumaanisha mpango wa wokovu mzima.

Hivyo, tunaona katika Matendo 2:38 "*Petro akawajibu*: *Tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu abatizwe kwa jina la Yesu Kristo, ili mpate kusamehewa dhambi zenu. nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu"*. Katika Matendo 10:43, Petro akamwambia "*Manabii wote walishuhudia juu yake kwamba kila mtu amwaminiye hupokea msamaha wa dhambi katika jina lake.*" Katika kifungu cha kwanza, Mtume anasema kwamba msamaha wa dhambi unapatikana kwa njia ya toba na ubatizo; katika kifungu cha pili, anasema kuhusu imani kwa namna ya ujumla: yaani toba na ubatizo ni hizo hatua zilizotajwa wazi katika Matendo 2:38.

Wale ambao, katika siku ya Pentekoste waliokubali ujumbe wa Petro, walibatizwa, kulingana na Matendo 2:41. Lakini aya ya 44 inazungumzia watu hawa ikisema "*Walioamini wote walikuwa mahali pamoja nao, walikuwa na kila kitu ushirika.*" Ni dhahiri kwamba, maelezo ya "walioamini" katika mstari wa 44 ni lazima ieleweke kwa maana ya wale ambao walikuwa wamebatizwa katika mstari wa 41. *"… Krispo, akamwamini Bwana pamoja na wote wa nyumbani mwake…"* (Matendo 18:8). Lakini kulingana na 1 Wakorintho 1:14 (*Namshukuru Mungu kwamba sikumbatiza mtu ye yote miongoni mwenu isipokuwa Krispo na Gayo.*), Krispo akabatizwa. Ni dhahiri kwamba, tendo hili la utiifu, lilijumlishwa katika kusema kwamba Krispo akamwamini Bwana.

Askari wa gereza mufilipi alibatizwa kadiri tunavyosoma katika aya ifuatayo: "*Wakati ule ule, yule mkuu wa gereza akawachukua akawaosha majeraha yao, kisha akabatizwa yeye pamoja na wote waliokuwa nyumbani mwake bila kuchelewa.*" (Matendo 16:33). Kwenye mstari wa 34 tunasoma, "*Akawapandisha nyumbani mwake akawaandalia meza mbele yao, yeye pamoja na wa nyumbani mwake wote wakafurahi sana kwa kuwa amemwamini Mungu.*" Hapa tena, "imani" ni pamoja na kitendo cha utii katika « ubatizo ».

Katika kila pahali panapotajwa wokovu katika kitabu cha Matendo ya Mitume (kitabu cha mifano ya wokovu), tunaona kwamba imani inadhihirishwa katika utiifu, inaambatana na mapenzi ya Bwana. Hakuna hata tofauti moja.

**76, Av. Industrielle, Bukavu – RDC.**
**Tel :** +243813148619
+243853163500
**Email :** klk.bukavu@yahoo.fr

Kwa kuhitimisha somo hili, tunatoka kuona kwamba imani katika Kristo, njiya pekee ya kuufikiya wokovu, inathibitishwa kupitiya hatua zifuatazo, tunapolinganisha na ingine mifano ya wale walioukubali wokovu katika Kristro:

a. Kusikia Neno la Mungu yaani Habari njema na liguse moyo: Rum. 10:17; Mdo. 2:37.
b. Kuamini Neno hilo ambalo linatuita kwenye wokovu: Mdo. 4:4; . 11:6; Heb. 10:14
c. Kutubu, yaani kuamua kubadili maisha (mafikiri na nia ao kuacha njia mbaya) maana yake roho huzaliwa upya na kuacha matendo ya zamani yasiyopendeza Mungu. Mdo. 2:38; Mdo. 17:3.
d. Kukiri Kristo kama Mwana wa Mungu aokowaye peke yake. (Mdo. 9: 37; Rum. 10: 9-10).
e. Kubatizwa kwa ubatizo halali wa kibiblia na kuongezwa na Bwana katika Kanisa lake. Mko. 16-16; Mdo. 8:38.

Somo mbili zitakazofuata, zi tatufundisha kwa kirefu kuhusu toba kwa jina la Kristo na ubatizo.

✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧☆☆☆☆☆☆☆☆✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧✧

Ikiwa una maswali yoyote wala kutaka mwangaza wa zaidi,

✍Andikiya:

- Kanisa la kristo pa Bukavu, SLP/Po Box: 222, Cyangugu-Rwanda.
- Email: klk.bukavu@yahoo.fr

⇨ Kutana na watumishi wa Mungu pahali wanaposhiriki pamoja na kanisa kwenye anuani ifuatayo:
N°76, Av. Industrielle, Bukavu – DRC.